

# JARIDA LA RS RUVUMA






## TOLEO LA AGOSTI 2024

www.ruvuma.go.tz



# KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigachapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

## JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA MWEZI AGOSTI 2024

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

## YALIYOMO

1.Tamasha la utamaduni la kitaifa kufanyika Songea Septemba
2.DED Namtumbo aunda timu ya ufutiliaji miradi
3.Halmashauri Mbinga yakusanya bilioni 7.7
4.Nyasa yakusanya mapato kwa asilimia 124
5.Marufuku kutoa huduma ya maji saa nane usiku
6.Ufahamu ugonjwa wa MPOX
7.Askofu aonya rushwa kwenye uchaguzi
8.Asilimia 97 ya huduma za matibabu ya nje zinapatikana nchini
9.RUWASA Nyasa yakabidhiwa gari jipya
10.Rais atoa mabilioni ya fedha kutekeleza miradi Songea
11.Abate mpya wa Peramiho asimikwa
12.TAKUKURU Ruvuma yawafunda wanahabari
13.Bandari za Ndumbi na Mbambabay kuinua uchumi wa Ruvuma
14.TAMISEMI yatoa pikipiki kwa watendaji Nyasa
15.Jiwe la Mbuji lilivyofungua utalii Mbinga
16.Ruvuma yakipanga kukabiliana na MPOX
17.Serikali yatoa bilioni 244 kutekeleza miradi Tunduru
18.Wakandarasi Tunduru waaswa miradi yenye ubora
19.TAKUKURU Ruvuma yabaini mapungufu kwenye miradi
20.RC Ruvuma asikiliza na kutatua kero za wananchi Tunduru
21.Kaya 76,000 Songea zapewa dawa za usubi na minyoo
22.Ruvuma yafanya tathmini ya lishe
23.Milioni 276 zanunua mashine ya meno HOMSO
24.Naibu Waziri azindua kituo cha mauzo ya makaa ya mawe
25.Utalii wa utamaduni unavyokuza utalii Nyasa
26.Wakulima Namtumbo wataja changamoto ya elimu ya mahindi
27.Wakulima Kigonsera wahimizwa usafi kwenye mahindi
28.Tunduru wauza mbaazi kilo 2,478,000
29.Malori 120 hubeba makaa ya mawe kwa siku mgodi wa Jitegemee

30.Utalii Nyasa unaanzia Mbambabay
31.Ziwa Nyasa lina aina 600 za samaki
32.Mwenyekiti Madabaakumbusha wataalam kujibu hoja
33.Naibu Waziri wa Habari asikiliza kero za mawasiliano Madaba
34.Bado vijiji viwili kati ya 544 Ruvuma kupata umeme
35.Waziri Jenista Mhagama akabidhiwa Ofisi
36.TIC yatoa semina kwa wafanya baishara Songea
37.Uchaguzi serikali za mitaa kufanyika Novemba 27
38.RC Ruvuma afanya mazungumzo na Kamishina wa TIRA
39.Mji wa Peramiho unavyoutangaza Mkoa wa Ruvuma kimataifa
40. Mito iliyogeuka mawe inavyovutia watalii Tunduru
41.Jenista Mhagama anavyoendelea kuaminiwa na Rais
42.SUPERFEO alianza na mtaji wa sh.20,000 sasa ni Mwekezaji mkubwa
43.Mwenyekiti CCM akabidhi vifaa tiba hospitali ya Nyasa
44.Kanali Abbas afungua kikao cha ukusanyaji maoni Dira mpya
45.TIRA yatoa elimu ya Bima kwa watumishi RS Ruvuma
46.Kanali Abbas afunga maonesho ya nanenane Ruvuma
47.Namtumbo washauriwa kuongeza bidii kwenye ufundishaji
48.Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yana mchango kwenye maendeleo

## TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.
Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wanavyosikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## TAMASHA LA UTAMADUNI LA KITAIFA KUFANYIKA SEPTEMBA UWANJA WA MAJIMAJI SONGEA



TAMASHA la Utamaduni la Kitaifa la tatu linatarajia kufanyika kwenye uwanja wa Majimaji mjini Songea mkoani Ruvuma mwezi Septemba mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Tamasha hilo Joel Mbewa amesema tamasha la kwanza la kitaifa la utamaduni lilifanyika mkoani Dar es salaam mwaka 2022 na tamasha la pili lilifanyika mkoani Njombe mwaka 2023.

Amesema katika matamasha hayo mawili ya kitaifa Mkoa wa Ruvuma ulifanikiwa kushika nafasi ya sita kitaifa kati ya mikoa 31 ya Tanzania Bara na visiwani.

“Kwa kuwa tamasha hili mwaka huu kitaifa linafanyika mkoani Ruvuma,tumedhamiria kufanya vizuri Zaidi ikiwezekana kushika nafasi ya kwanza kitaifa kati ya mikoa 31 inayoshiriki kwenye tamasha hilo’’,alisisitiza.

Tamasha la kitaifa la utamaduni lilianzishwa mwaka 2022 ikiwa ni kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa alipokuwa mgeni rasmi mkoani Mwanza Septemba 8,2021 katika Tamasha la utamaduni la Bulabo.

Rais Samia aliagiza matamasha ya utamaduni kufanyika kwa mzunguko kila Mkoa ili watanzania wajue mila na desturi za kila Mkoa ambapo aliagiza kuwe na mashindano ya ngoma za asili na washindi wapewe Tuzo.

Malengo makuu ya tamasha la kitaifa la utamaduni ni kurithisha amali za utamaduni kwa vitendo, kuchochea maendeleo ya utalii wa kiutamaduni, Sanaa za

asili,sekta za ubunifu wa asili, kuhamasisha utaifa,uzalendo na urithishaji wa maadili kwa mtanzania

## DED NAMTUMBO AUNDA TIMU YA UFUATILIAJI MIRADI



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma Philemon Magesa ameunda timu itakayohusika na Ufuatiliaji na kufanya tathmini ya miradi mbalimbali kabla ya Kufanya Malipo kwa Mkandarasi, Fundi au Mzabuni.

Akizungumza Katika kikao kazi na watendaji kutoka katika kata 21 za Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kilichofanyika mjini Namtumbo,Magesa amewataka watendaji kata Kuwa makini katika usimamiaji na ufuatiliaji wa miradi katika kata zao.

Amesema uwepo wa timu hiyo itasaidia kufanya Malipo kwa Mkandarasi, Fundi au Mzabuni aliye kidhi vigezo vya mahitaji ya Halmashauri hiyo na kwamba timu itahakikisha miradi inatekelezwa kwa viwango.

Amesema timu hiyo pia itaangalia vifaa na mahitaji yanayonunuliwa kama yapo katika mpango wa mradi huo ili Mkandarasi, Fundi au Mzabuni aweze kulipwa Stahiki kihalali.

## HALMASHAURI MBINGA YAKUSANYA SHILINGI BILIONI 7.7



Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma imevuka lengo katika ukusanyaji wa mapato kwa kukusanya Zaidi ya shilingi bilioni 7.76 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani katika mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu CPA. Samwel Marwa katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani kujadili taarifa za hesabu za Halmashauri kilichofanyika katika Halmashauri hiyo.

Amesema, katika mwaka huo wa fedha Halmashauri hiyo iliidhinishiwa kukusanya shilingi 6,300,000,000 ambapo hadi kufikia Februari kiasi cha shilingi 5,050,776,560.11 kilikusanywa sawa na asilimia 80 ya makusanyo.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas akikagua mabanda ya maonesho katika maadhimisho ya Sikukuu ya wakulima Nanenane ngazi ya Mkoa yaliyofanyika katika viwanja vbbya Amanimakoro wilayani Mbinga

# HALMASHAURI NYASA YAKUSANYA MAPATO KWA ASILIMIA 124



Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma imevuka lengo la ukusanyaji mapato,baada ya kufanikiwa kukusanya mapato ya zaidi ya shilingi bilioni 2.17 sawa na asilimia 124.91 katika kipindi cha mwaka 2023/2024.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Khalid Khalif kwenye kikao cha Baraza la madiwani cha kujadili taarifa ya Hesabu za mwisho za Halmashauri kwa mwaka wa fedha za 2023/2024 kilichofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkurugenzi Kilosa Mbambabay.

Amebainisha kuwa kati ya makusanyo hayo,mapato halisi ni shilingi bilioni 1.32 na mapato kutoka katika vyanzo zuiliwa ni zaidi ya shilingi milioni 859.

“Fedha za miradi ya maendeleo ambazo zimepokelewa katika kipindi hicho ni 11,857,058,019 ambazo zimetumika kwa ajili ya mfuko wa afya wa Pamoja,elimu bure, TASAF, SEUIP, P4R, UNICEF,CDCF,chanjo ya polio, umaliziaji wa maboma, shule shikizi,BOOST na swash’’,alisema.

Ameongeza kuwa mapato kutokana na kodi mbalimbali katika kipindi hicho yameongezeka kutoka shilingi 202,319,610 kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia shilingi 271,856,574 mwaka 2023/2024.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Peres Magiri akizungumza kwenye kikao hicho ameagiza kufanyika vikao vya kamati ya afya ngazi ya wilaya ambavyo vinazungumzia suala zima la afya kwa ujumla ikiwemo kutambua suala zima la virusi vya UKIMWI na vifo vya mama na mtoto.

Mkuu wa Wilaya pia ameagiza ratiba ya vikao vya lishe ngazi ya Halmashauri iandaliwe na kuhakikisha vikao vinafanyika kwa wakati ili kutekeleza mikataba ya lishe katika ngazi zote hadi Kata ili kukabiliana na udumavu.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Stewart Nombo amewapongeza watumishi na waheshimiwa madiwani wa Halmashauri hiyo kwa kusimamia ukusanyaji wa mapato hali iliyosababisha kuvuka malengo ya makusanyo kwa asilimia zaidi ya 124.

Baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa lina madiwani wa kuchaguliwa 20,viti ,maalum madiwani saba na Mheshimiwa mbunge mmoja.

## MARUFUKU KUTOA HUDUMA YA MAJI SAA NANE USIKU



Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso amepiga marufuku kwa Mamlaka zote za maji nchini kuacha tabia ya kutoa huduma za maji saa nane za usiku.

"Unatoa maji saa nane za usiku afanye nini mwananchi,Katibu Mkuu upo hapa waambie kabisa watendaji wako,huduma ya maji itolewe muda ambao mwananchi

anaweza kupata ile huduma bila usumbufu wa aina yoyote'', alisisiza Waziri wa Maji.

Hata hivyo amesema iwapo kuna hitilafu ya kusababisha huduma ya maji kutopatikana ni vema wananchi wafahamishwe mapema,ambapo amekemea tabia ya kukata maji siku nzima bila kutoa taarifa kwa wananchi hivyo kutengeneza manung'uniko yasiyokuwa ya lazima kwa wananchi.

Amekiagiza Kitengo cha Mawasiliano kwenye Mamlaka za maji kutoa taarifa kwa wakati kwa wananchi ili wafahamu mapema na kujipanga namna ya kuhifadhi maji.



Wizara ya Afya

# FAHAMU DALILI ZA UGONJWA WA MPOX



Upele, malengelenge au vidonda kwenye mwili hasa mikononi na miguuni, kifuani, usoni wakati mwingine sehemu za siri



Homa




maumivu ya kichwa



maumivu ya misuli



uchovu wa mwili



Maumivu ya mgongo



Kuvimba mitoki ya mwili



vidonda vya koo

Wahi katika kituo cha huduma za afya kwa uchunguzi na matibabu unapoona mojawapo ya dalili za Ugonjwa wa Mpox

*"Afya Yangu, Mtaji Wangu"*

World Health Organization unicef

*"Kwa Taarifa, Elimu na Ushauri piga 199 BURE"*

Elimu ya Afya Tovuti: www.moh.go.tz

# JINSI YA KUJIKINGA NA UGONJWA WA MPOX



Epuka kugusa majimaji ya mwili ya mtu mwenye maambukizi ya Ugonjwa wa Mpox



Epuka kusalimiana kwa kukumbatiana, kubusiana au kushikana mikono na mtu mwenye maambukizi ya Mpox



Epuka kugusana na mtu mwenye dalili za Ugonjwa wa Mpox



Nawa mikono yako mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au tumia vitakasa mikono



Epuka kula au kugusa mizoga au wanyama pori wenye maambukizi ya Ugonjwa wa Mpox



Epuka kusogeleana karibu na mtu mwenye dalili za Mpox wakati mnaongea



Epuka kugusa vyombo, matandiko, nguo au godoro la mtu mwenye Ugonjwa wa Mpox



Vaa barakoa ikiwa unaongea kwa karibu na mtu aliye na dalili za ugonjwa huo



Unapo kohoa au kupiga chafya ziba mkono kwa kiwiko



Safisha na takasa sehemu zote na vitu ambavyo vinaguswa mara kwa mara

Wahi katika kituo cha huduma za afya kwa uchunguzi na matibabu unapoona mojawapo ya dalili za Ugonjwa wa Mpox

*Fanya Kweli Usibaki Nyuma Mtu ni Afya*

Wizara ya Afya

World Health Organization unicef

*"Kwa Taarifa, Elimu na Ushauri piga 199 BURE"*

Elimu ya Afya Tovuti: www.moh.go.tz

Wizara ya Afya

# JINSI YA KUJIKINGA NA UGONJWA WA MPOX

- Epuka kugusa majimaji ya mwili Wa mtu mwenye maambukizi ya Mpox
- Epuka kusalimiana kwa kukumbatiana, kubusiana au kushikana mikono na mtu mwenye maambukizi ya Mpox
- Epuka kugusana na mtu mwenye dalili za Ugonjwa wa Mpox
- Nawa mikono yako mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au tumia vitakasa mikono
- Epuka kula au kugusa mizoga au wanyama pori wenye maambukizi ya Ugonjwa wa Mpox
- Epuka kusogeleana karibu na mtu mwenye dalili za Mpox wakati mnaongea
- Epuka kugusa vyombo, matandiko, nguo au godoro la mtu mwenye Ugonjwa wa Mpox
- Vaa barakoa ikiwa unaongea kwa karibu na mtu aliye na dalili za Mpox
- Unapo kohoa au kupiga chafya ziba mkono kwa kiwiko
- Safisha na takasa sehemu zote na vitu ambavyo vinaguswa mara kwa mara
- Epuka kujamiiana na mtu mwenye maambukizi ya ugonjwa huo

Wahi katika kituo cha huduma za afya kwa uchunguzi na matibabu unapoona mojawapo ya dalili za Ugonjwa wa Mpox


*"Afya Yangu, Mtaji Wangu"*

World Health Organization unicef

*Kwa Taarifa, Elimu na Ushauri piga 199 BURE"*

Elimu ya Afya Tovuti: www.moh.go.tz

## ASKOFU MKUU AONYA KUEPUKA RUSHWA KWENYE UCHAGUZI



Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Songea Mhashamu Damian Dallu ametoa onyo kali kwa jamii na viongozi juu ya masuala ya rushwa katika uchaguzi na matumizi mabaya ya madaraka.

Mhashamu Dallu ametoa onyo hilo wakati anahubiri kwenye adhimisho la misa takatifu ya kumsimika na kumbariki Abate mpya wa Peramiho, Mhashamu Emanuel Mlwilo OSB iliyofanyika katika Kanisa la Abasia ya Peramiho Jimbo Kuu la Songea.

"Inawezekana tatizo halipo kwa watu hawa wanaochaguliwa, Sasa rushwa imeingia katika jamii, bila kupokea rushwa hakuna raha, mtakosa wale ambao wanataka wawasaidie" alisisitiza Mhashamu Dallu.

Amekemea tabia ya rushwa licha ya kwamba ni dhambi na kwamba inaathiri uchaguzi, na kuchangia kuleta viongozi wasiofaa ambao hawana nia ya kutumikia jamii bali kufaidika kwa kutoa rushwa.

Ameonya kuwa kuendeleza tabia ya kupokea rushwa itaiumiza serikali kwa kuwa italeta viongozi wasiofaa, ambao hawawezi kuwatumikia watu bali kuwanufaisha viongozi wanarushwa.

Katika hatua nyingine Askofu Mkuu Dallu amewasihi viongozi wa dini na wale wenye mamlaka serikalini kutotumia vibaya madaraka yao badala yake wawe wanyenyekevu na kuwatumikia wale waliowachagua.

Kauli ya Askofu Dallu imekuja wakati ambapo jamii inajiandaa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika nchini Novemba 27,2024 na uchaguzi mkuu wa Rais,wabunge na madiwani ambao unatarajia kufanyika mwaka 2025.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo akizungumza kwenye majumuisho ya maonesho ya nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini viwanja vya John Mwakangale ambapo ameahidi kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ikiwemo kuboresha mabanda ya maonesho ya Halmashauri zote nane ili yaendane na hadhi ya kikanada,kitaifa na kimataifa.

## ASILIMIA 97 YA HUDUMA ZA MATIBABU ZA ULAYA NA INDIA SASA ZINAPATIKANA NCHINI



Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dr. Godwin Mollel, ameeleza mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta ya afya.

Akizungumza wakati wa ibada ya kumsimika Abate mpya wa Peramiho iliyofanyika katika Kanisa la Peramiho, Dr. Mollel amesema kuwa kwa asilimia 97, serikali imewezesha huduma za kiteknolojia za afya zinazotolewa Ulaya na India kupatikana katika hospitali zilizopo hapa nchini.

"Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye sekta ya afya amefanya uwekezaji mkubwa, ameshakamilisha asilimia 97 ya teknolojia tuliyokuwa tunaifuata Ulaya na India tayari iko kwenye nchi yetu," alieleza Dr. Mollel

Naibu waziri ameitaja teknolojia hiyo kuwa na uwezo wa kurahisisha huduma za upasuaji kama vile uvimbe chini ya sakafu ya ubongo, kifua, moyo, mgongo, na huduma kwa watoto wanaozaliwa na seli mundu ambapo huduma zote hizo sasa zinatolewa nchini.

Sanjari na hayo Naibu Waziri ameeleza umuhimu wa lishe bora katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ambayo inaongoza kwa uzalishaji wa chakula lakini inakabiliwa na tatizo la lishe na udumavu.

Ametoa wito kwa viongozi wa dini kuwasaidia wananchi kutambua umuhimu wa lishe bora ili kuimarisha afya ya jamii na kuweza kuchangia maendeleo katika Taifa.

## RUWASA WILAYA YA NYASA WAKABIDHIWA GARI JIPYA




Mkuu wa Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma Mhe. Peres Magiri, amekabidhi gari jipya kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Nyasa gari lililotolewa na Wizara ya Maji kwa lengo la kutatua kero ya usafiri kwa mamlaka hiyo.

Hafla ya makabidhiano ya gari hilo imefanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyasa na kuhudhuriwa na watumishi pamoja na wananchi wa Wilaya ya Nyasa.

Ameishukuru Serikali kwa kuipa Wilaya ya Nyasa gari ambalo linakwenda kutoa huduma ya usafiri wa uhakika na kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama.

Malengo ya Serikali, ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025, wananchi wote waishio Vijijini katika Mkoa wa Ruvuma, wanafikiwa na kupata huduma ya maji safi na salama kwa asilimia 85 na ifikapo 2030 wanapata huduma maji kwa asilimia 100.

# RAIS ATOA MABILIONI YA FEDHA KUTEKELEZA MIRADI SONGEA



MSTAHIKI Meya Manispaa ya Songea mkoani Mheshimiwa Michael Mbano Ruvuma amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu kwa kuleta fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Manispaa hiyo.

Mbano amesema Manispaa ya Songea imeendelea kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo ikiwemo na mradi wa barabara wenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 22 na mradi wa mitaro ya maji wenye thamani ya shilingi bilioni. 157.



Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na Chuo cha Utumishi wa Umma, imetoa mafunzo maalum kwa Maafisa Tarafa na Maafisa Watendaji wa Kata katika Mkoa wa Ruvuma

Mafunzo hayo yanatolewa kwa siku mbili katika Ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, yakilenga kuwawezesha viongozi hao kuboresha utendaji kazi wao wa kila siku kwa kuzingatia sheria, taratibu, na miongozo ya serikali.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo hayo amewataka maafisa tarafa na watendaji kata kushughulikia kero za wananchi kwa haraka akiwasisitiza umuhimu wa kujenga uwezo wa kutatua matatizo yanayowakabili wananchi katika maeneo yao.

"Nilazima tujenge Hali ya umiliki kwa kazi tulizopewa, na baada ya kujenga hiyo hali ya umiliki ni lazima tusikilize na kutatua kero za wananchi ili watuone sisi ni msaada kwao na watukimbilie'',alisisitiza.

Ameongeza kuwa uzoefu unaonesha kuwa zimekuwepo changamoto nyingi ambazo zinaathiri utoaji wa huduma kwa wananchi katika ngazi ya kata na tarafa zinazotokana na kutokuzingatiwa kwa kanuni, sheria na taratibu katika utendaji kazi.

Mshiriki wa mafunzo hayo ambaye ni Afisa Tarafa wa Peramiho Salma Mapunda, amesema mafunzo hayo yatawajengea uwezo na kuwakumbusha utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo usimamizi wa miradi na usimamizi wa ununuzi ndani ya tarafa.

Ameongeza kuwa mafunzo hayo yatawaongezea uwajibikaji ili kuleta maendeleo na kutatua kero za wananchi kwa kusimamia utawala bora wenye uwazi na Uwajibikaji

Ofisi ya Rais TAMISEMI hadi sasa tayari imeshatoa mafunzo hayo kwa mikoa 20 kati ya 26 ya Tanzania Bara.

## ABATE MPYA WA ABASIA YA PERAMIHO ASIMIKWA



Naibu Waziri wa Afya Dr.Godwin Mollel amemwakilisha Waziri wa Afya na Mbunge wa Peramiho Mheshimiwa Jenista Mhagama katika sherehe za kumsimika na kumbariki Abate mpya wa Abasia ya Peramiho Mhashamu Emanuel Mlwilo ndani ya kanisa la Abasia ya Peramiho Jimbo Kuu Katoliki la Songea



## SHEREHE ZA KUMSIMIKA ABATE MPYA WA PERAMIHO



Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ambaye pia ni Mkuu wa wilaya ya Songea Mheshimiwa Kapenjama Ndile akızüngumza ndani ya kanisa la Abasia ya Peramiho Songea mkoani Ruvuma kwenye sherehe za kusimikwa kwa Abate mpya wa Abasia ya Peramiho Mhashamu Emanuel Mlwilo OSB leo Agosti 24,2024.Adhimisho la Misa takatifu ya kusimikwa na kumbariki Abate mpya wa Peramiho imeongozwa na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Songea Mhashamu Damian Dallu.



# TAKUKURU RUVUMA YAWAFUNDA WANAHABARI




MIONGONI mwa madhara makubwa ya rushwa kwenye uchaguzi yametajwa kuwa ni kunyima haki ya kuchagua kiongozi bora na anayehitajika hivyo kukwamisha maendeleo kutokana na viongozi waliopatikana kwa njia ya rushwa.

Hayo yamesemwa na Afisa wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma Yahaya Mwinyi wakati anatoa mada ya nafasi ya wanahabari katika mapambano ya rushwa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 2024 na uchaguzi Mkuu 2025.

TAKUKURU wameandaa mafunzo hayo kwa wanahabari 21 kutoka vyombo mbalimbali vya Habari wilayani Songea ambayo yamefanyika kwenye ukumbi wa TAKUKURU Mahenge Manispaa ya Songea.

Mwinyi ameyataja madhara mengine ya rushwa kwenye uchaguzi kuwa ni wananchi wanadharirika kwa kuthaminishwa na vitu vidogo kama pombe na zawadi ili kuwachagua viongozi wasiokuwa na sifa hivyo jamii kukosa huduma muhimu kama zahanati,umeme na maji.

“Madhara ya rushwa kwenye uchaguzi,wananchi kupata viongozi wasiokuwa waadilifu na kuongezeka kwa umasikini kwa sababu viongozi waliochaguliwa wanakosa sifa za kuwaletea maendeleo wananchi’’.alisisitiza Mwinyi.

Awali akizungumza kwenye ufunguzi na ufungaji wa mafunzo hayo Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma Janeth Haule amesema TAKUKURU imeamua kufanya mafunzo hayo kwa wanahabari kwa kutambua Taifa linaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Amesema wanahabari wana mchango mkubwa katika mapambano dhidi ya rushwa kwa sababu wanahabari ni kioo cha jamii na wana uwezo mkubwa wa kuwafikia wananchi wengi kwa haraka.

“Vyombo vya Habari vinaaminika sana kwa wananchi kwa hiyo tumeona tuanze kutoa mafunzo haya kwanza kwa wanahabari na baadaye tutaingia katika makundi mengine’’,alisema Haule.

Amesisitiza kuwa vyombo vya Habari vina nafasi kubwa ya kuzuia rushwa kwenye uchaguzi hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

Ameutaja wajibu wa vyombo vya Habari hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa ni kubadili fikra za wananchi kulingana na misingi ya maadili,uadilifu,utawala bora,haki za binadamu,uzalendo na upendo.

TAKUKURU Ruvuma itaendelea na uelimishaji wa madhara ya rushwa kwenye uchaguzi kwa kutoa elimu katika makundi mbalimbali yakiwemo wanahabari,viongozi wa dini,viongozi wa vyama vya siasa na kuendelea kuwaelimisha wananchi kwa ujumla kuhusu mapambano dhidi ya rushwa kuelekea kwenye uchaguzi .




MWAKILISHI wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mheshimiwa Kapenjama Ndile katikati akiwa na viongozi wengine wa Mkoa wa Ruvuma na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa ujumla walipotembelea banda la Chuo Kikuu Huria ch Tanzania kwenye maonesho ya nane nane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini viwanja vya John Mwakangale Mbeya

# BANDARI ZA NDUMBI NA MBABABAY ZITAKAVYOFUNGUA FURSA ZA KIUCHUMI




Ujenzi wa bandari za Ndumbi na Mbambabay ziwa Nyasa wilayani Nyasa mkoani Ruvuma utatoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuimarisha uhusiano wa kijamii kati ya Tanzania na nchi jirani

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakati anazungumza na wanahabari ofisini kwake mjini Songea.

Amesema bandari hizo ni sehemu muhimu ya mpango wa kitaifa wa kutengeneza ushoroba wa Mtwara, ambao unatarajiwa kuchochea maendeleo katika mkoa wa Ruvuma na maeneo mengine nchini

Amezitaja nchi za Malawi na Msumbiji kuwa zitanufaika na kwamba bandari hizo zitaongeza uhusiano wa kijamii na kiuchumi kati ya nchi hizo na kuimarisha zaidi uhusiano wa kimataifa.

" Bandari hizi zitawezesha usafirishaji wa abiria kati ya nchi hizo na kusaidia katika masuala ya kiuchumi na maendeleo kwa ujumla.

Kanali Abbas amesema bandari hizo zitafungua milango kwa nchi jirani kutumia miundombinu ya Tanzania kusafirisha bidhaa na kuwezesha usafirishaji wa makaa ya mawe yanayozalishwa kwa wingi mkoani Ruvuma.

Amesema katika utekelezaji wa miradi hiyo,watanzania wanapata faida kubwa ikiwemo kuongeza ajira na kuimarisha uchumi wa mwananchi mmoja mmoja, mkoa na Taifa kwa ujumla

Mkoa wa Ruvuma umebarikiwa kuwa rasilimali nyingi yakiwemo madini,hivyo kuwa na miundombinu ya kisasa kama bandari, uwanja wa ndege, na barabara za kuaminika kunatoa fursa kwa wawekezaji kuwekeza hali inatakayochochea maendeleo na kukuza uchumi.

## TAMISEMI YATOA PIKIPIKI KWA WATENDAJI NYASA




Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma imekabidhi pikipiki kwa watendaji wa Kata tatu za Mpepo,Mbambabay na Liwundi ili kuongeza uwajibikaji kwa wananchi.

Pikipiki hizo zimekabidhiwa kwa watendaji hao na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nyasa Khalid Khalif amewataka watendaji hao wafanye kazi kwa juhudi na kuongeza uwajibikaji kwa wananchi,ikiwa ni Pamoja na kutatua kero za wananchi.

Pikipiki hizo zimetoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI na zimeletwa kwa ajili ya watendaji hao ili waweze kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi.

Amemshukuru Mhe. Dkt Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa usafiri wa Pikipiki hizo.

Wakizungumza baada ya kukabidhiwa pikipiki hizo,Hiram Malugu ni Mtendaji Kata ya Mbamba bay ambaye amesema alikuwa anatumia pesa ya mfukoni kwa ajili ya kwenda kutatua changamoto za wananchi.

## JIWE LA MBUJI LILIVYOFUNGUA FURSA YA UTALII MBINGA



MKOA wa Ruvuma una vivutio vingi tofauti ambavyo bado havitumiki katika kuchangia pato la Taifa na kuinua uchumi wa wananchi wa eneo husika.

Jiwe la Mbuji ambalo lipo katika wilaya ya Mbinga ni miongoni mwa vivutio adimu na vya kipekee vilivyopo katika Bonde la ziwa Nyasa ambalo linajumuisha mikoa ya Mbeya,Ruvuma na Njombe.

Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Africanus Challe anasema tayari Idara yake imeliingiza jiwe la Mbuji kwenye orodha ya vivutio vya utalii katika Mkoa wa Ruvuma ili hatimaye kazi ya kutangaza eneo hilo na vivutio vingine iweze kufanyika kwa tija.

Kivutio cha jiwe la Mbuji kimekuwa gumzo kwa wengi waliosikia taarifa za kivutio hicho.Neno Mbuji kwa lugha ya kabila la wamatengo ni **"Kitu kikubwa",**jiwe hili lipo katika kijiji cha Mbuji kata ya Mbujii na limekuwa kivutio adimu kwa wageni wa ndani na nje ya nchi.

Jiwe la Mbuji lina maajabu mengi yakiwemo jiwe pekee kubwa Mkoani Ruvuma,lina vyanzo vingi vya maji chini yake,ni vigumu kulipanda bila kuwaona wazee kwa sababu ni vigumu kupanda na kulizunguka jiwe hilo bila kufuata mila na desturi za kabila la wazee wa kimatengo.

Unapofika katika jiwe hilo inakulazimu kuwatafuta wazee wanaotoa maelekezo kwa yeyote anayetaka kupanda jiwe hilo,ambalo linaheshimika sana na wakazi wanaolizunguka jiwe hilo.

Ili kupanda jiwe hilo ni lazima uwe na Mwongozaji ambaye ni mzee wa mila ambaye anazifahamu vizuri mila na taratibu za kabila la wamatengo zitakazokuwezesha kupanda jiwe hilo bila matatizo na kufurahia vivutio vilivyopo.

Historia inaonesha kuwa jiwe ka mbuji tangu zamani lilikuwa linatumiwa na wazee kwa ajili ya kutambika katika mila na desturi kwa kufuata mila na desturi ikiwemo kutumia unga wa mhogo na kujipaka kabla ya kuanza kupanda jiwe hilo.

"Iwapo mtalii ataamua kupanda jiwe hilo bila kuwaona wazee wa mila na desturi atakuwa amevunja mila na desturi na anastahili kupata adhabu na hata kushindwa kulizunguka jiwe hilo", anasisitiza Ndunguru.

Ili kulimaliza jiwe hilo kulizunguka inachukua kati ya saa 12 hadi 14 ingawa muonekana wake kwa macho unaweza kulimaliza kulizunguka jiwe hilo hata kwa nusu saa tu.

Jiwe la Mbuji pia hutumika kuwaombea watu wanaosumbuliwa na mapepo ambao hupandishwa juu ya jiwe hilo na kuombewa kimila na kwamba inaaminika mapepo hayo huondoka na wagonjwa wa mapepo wanakuwa wamepona kabisa wanaposhuka chini ya jiwe hilo.

Kutokana na maajabu hayo Ndunguru anasema ndiyo maana jiwe hilo linaitwa jiwe la maajabu ambayo yanavutia wengi.

Uchunguzi umebaini kuwa unapoliangalia jiwe la mbuji kwa mbali linaonekana kwamba ni fupi lakini kadri unavyolikaribia ndivyo jiwe hilo linavyoonekana kuwa refu na kuwa na ugumu kulizunguka lote kwa muda mfupi.



BAADHI ya wakurugenzi watendaji wa Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma na watumishi wengine wakiwa kwenye kikao cha majumuisho ya maonesho ya nanene Nyanda za Juu Kusini kilichoongozwa na Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mheshimiwa Kaapenjama Ndile ndani ya viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya

## MKOA WA RUVUMA ULIVYOJIPANGA KUKABILIANA NA MPOX



Mkoa wa Ruvuma unaendelea kuchukua hatua madhubuti za kupambana na ugonjwa wa homa ya nyani (Mpox).

Hayo yameelezwa na Mratibu wa Huduma za Chanjo Mkoa wa Ruvuma Winbroad Mvile kwenye kikao cha tathmini ya lishe, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Mvile ameutaja ugonjwa wa Mpox kuwa unasababishwa na virusi ambavyo kwa sasa havina tiba, na njia pekee ya kupambana nao ni kuchukua tahadhari za kujikinga, ikiwemo kuepuka kugusana na wanyama au watu waliopata maambukizi.

"Mkoa wa Ruvuma umechukua hatua kadhaa kupambana na kuzuia Ugonjwa wa Mpox halmashauri zote za Mkoa zimeagizwa kujiandaa dhidi ya ugonjwa wa Mpox'', alisema.

Hata hivyo amesema timu za ufuatiliaji wa Mpox zinafanya ufuatiliaji ili kufahamu kama Kuna dalili za uwepo wa ugonjwa huu katika mkoa wa Ruvuma.

Amebainisha kuwa hadi sasa, hakuna mgonjwa yeyote aliyethibitishwa kuwa na maambukizi ya Mpox nchini ingawa nchi jirani kama Congo na Uganda tayari zimekuwa na visa vya ugonjwa huu

Amesema elimu juu ya ugonjwa wa Mpox na namna ya kujikinga nayo imeshatolewa katika taasisi za serikali na mikusanyiko mbalimbali, ili kuhakikisha jamii inatambua athari zake na namna ya kujikinga

Amebainisha kuwa halmashauri zote za mkoa wa Ruvuma zimetenga wodi maalum kwa ajili ya kuwahudumia waathirika wa Mpox, endapo watabainika.

Mpox ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Mpox ambapo awali ugonjwa huo ulijulikana kama ugonjwa wa monkey pox (ugonjwa wa nyani) na virusi hivi kwa kawaida ushambulia wanyama hususani nyani na panya.

## SERIKALI YATOA BILIONI 244 TUNDURU KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO



Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka miwili imetoa Zaidi ya shilingi bilioni 244 kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani Tunduru.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakati anazungumza na wananchi wa Tunduru kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya Baraza la Eid mjini Tunduru.

Amesema fedha hizo zinaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya hiyo ikiwemo miradi katika sekta ya elimu ambapo hivi sasa katika wilaya hiyo wanafunzi wote wanaofaulu kujiunga na kidato cha kwanza wanachaguliwa kwa kuwa Wilaya ina miundombinu ya vyumba vya madarasa vya kutosha.

“Kwenye sekta ya afya napo tumepiga hatua kubwa kwani wananchi wetu wanapata huduma ya afya vizuri katika hospitali ya Wilaya,vituo vya afya na zahanati zetu kwa ukaribu zaidi’’,alisisitiza.

Akizungumzia sekta ya kilimo,Kanali Abbas amesema serikali imeimairisha mfumo wa stakabadhi za ghala ambapo wakulima wanauza mazao yao kwa bei ambayo inamwezesha mkulima kurudisha gharama zake anazozitumia katika uzalishaji.

Hata hivyo amesema karibu sekta zote zikiwemo za umeme,maji,barabara za vijijini na mjini zinafanya vizuri kutokana na serikali kutoa fedha za kutekeleza miradi hiyo.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Dr.Wilfred Rwechungura amesema Halmashauri hiyo inaendelea kufanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na upungufu wa madarasa ,madawati,viti na meza za wanafunzi.

Hata hivyo amesema hadi sasa katika shule za sekondari Halmashauri haina upungufu wa vyumba vya madarasa,viti na meza,badala yake kuna upungufu wa madarasa na madawati katika shule za msingi.

Rwechungura amesema katika kukabiliana na changamoto hiyo,Halmashauri ya Wilaya imekuwa inatenga fedha kutoka vyanzo vya ndani na serikali kuu ili kujenga miundombinu ya shule ambapo kuanzia mwaka 2021 zaidi ya shilingi bilioni 2.5 zimetumika kujenga madarasa katika shule za msingi.

Kaimu Mkurugenzi huyo amesema kupitia mradi wa BOOST Halmashauri hiyo imeweza kupokea zaidi ya shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule za msingi.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma anafanya ziara ya kikazi katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma kwa lengo kuzungumza na wananchi ,kusikiliza kero zao na kupashana Habari za maendeleo zinazofanywa na serikali ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo.



Baadhi ya majengo katika hospitali ya Wilaya ya Tunduru.

# WAKANDARASI TUNDURU WAASWA KUJENGA MIRADI YENYE VIWANGO




MKUU wa wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma Simon Chacha,amewataka wakandarasi wanaotekeleza miradi ya barabara wilayani humo kuzitendea haki fedha zinazotolewa na Serikali kwa kujenga miradi yenye viwango itakayosukuma na kuharakisha shughuli za maendeleokwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Chacha amesema hayo,wakati akizungumza na watumishi wa TARURA na wakandarasi waliopata kazi za ujenzi wa miradi ya barabara zinazosimamiwa na wakala wa barabara za mijini na vijijini(TARURA)wilayani humo.

Chacha,amewaeleza wakandarasi hao kutekeleza kazi zilizoko kwenye mikataba waliyoingia na Serikali kupitia Tarura,kuwa wazalendo kwa nchi yao na kujenga miradi yenye viwango ambayo itachochea na kuharakikisha kukua kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja,wilaya na Taifa.

“Nendeni mkapige kambi kwenye maeneo ya miradi ili mpate muda mwingi utakaowawezesha kukamilisha kazi mlizopewa kwa wakati, wananchi wana matarajio makubwa na nyinyi, epukeni kuwa na visingizio vinavyoweza kuchelewesha ujenzi wa miradi”alisema Chacha.

Meneja wa TARURA wilaya ya Tunduru Silvanus Ngonyani amesema,kwa mwaka wa fedha 2024/2025 TARURA Wilaya ya Tunduru,imeidhinishiwa Sh.bilioni 4,110,783,784.47 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya fedha.
Kwa upande wake Mkuu wa Taasisi ya kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKU) Wilayani humo George Njoholo, amewataka wakandarasi kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa viwango ili iendane na gharama halisi ya fedha zilizotolewa na Serikali.

## TAKUKURU RUVUMA YABAINI MAPUNGUFU MIRADI YA BILIONI SABA




TAASISI ya kuzuia na kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma,katika kipindi cha miezi sita imefuatilia jumla ya miradi 31 yenye thamani ya Sh.bilioni 19,681,124,604.63 kati ya hiyo miradi mitano yenye thamani ya Sh.bilioni 7,053,240,916.51 imebainika kuwa na mapungufu.

Naibu Mkuu wa Takukuru mkoani Ruvuma Janeth Haule, ameitaja miradi iliyokutwa na upungufu ni ya sekta ya elimu,miundombinu na barabara na hatua mbalimbali zimechukuliwa na ili kuondoa mapungufu hayo.

Ameitaja miradi hiyo kuwa ni ujenzi wa soko katika Halmashauri ya Madaba wenye thamani ya Sh.milioni 171,176,339.00 ambapo bati 98 zimenunuliwa zaidi ya

mahitaji na manunuzi ya Terazo kinyume na taratibu za manunuzi.

Miradi mingine ni mradi wa maji Nangombo-Kilosa unaojengwa na Mkandarasi Contructions Of Gravity Pumping Water Supply kwa gharama ya Sh.bilioni 4.1 ambaye ameshindwa kuendelea na kazi kutokana na kuisha kwa mkataba kabla hajamaliza kazi.

Aidha mradi wa ukarabati wa Zahanati ya Litolomelo wenye gharama ya Sh.milioni 50 ambao kamati ya manunuzi na mapokezi zilifanya udanganyifu kwenye fedha za ukarabati na kupokea vifaa vya ujenzi wa mradi huo vikiwa pungufu.

Kwa mujibu wa Haule, mradi mwingine ni ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya msingi Nakawale Halmashauri Namtumbo wenye thamani ya Sh.milioni 80.

Amesema,ujenzi wa tanki la maji Mchomoro wilayani Namtumbo wenye thamani ya Sh. bilioni mbili ambapo miradi yote haijakamilika kwa muda uliopangwa.

## RC RUVUMA ASIKILIZA NA KUTATUA KERO ZA WANANCHI WA TUNDURU



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amefanya ziara ya kikazi ya siku moja wilayani Tunduru ambapo amefanya mkutano wa hadhara na

wananchi katika uwanja wa Baraza la Eid na kusikiliza kero 28 za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi,

Kabla ya kufanya mkutano na wananchi Mkuu wa Mkoa pia alifanya mkutano wa ndani na viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa,dini watalaam,waheshimiwa madiwani ,mkutano huo pamoja na mambo mengine pia ulilenga kusikiliza kero mbalimbali za wananchi wa Tunduru kupitia viongozi hao





kulia ni Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Kapenjama Ndile akikagua mabanda ya maonesho nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini jijini Mbeya ambapo alifanikiwa kukagua mabanda mbalimbali na kujionea bidhaa za wajasirimali wadogo kutoka Kanda hiyo

# KAYA 76,000 SONGEA ZAPEWA DAWA ZA USUBI NA MINYOO



Katibu Tawala Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma Mtela Mwampamba, amewataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa wataalamu wa afya katika zoezi la linaloendelea la umezeshwaji wa dawa za kinga tiba ya Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ikiwemo Usubi na Minyoo ya tumbo.

Zoezi hilo hufanyika kila mwaka Kitaifa chini ya Wizara ya Afya kwa kushirikiana na RTI, ambapo kwa Manispaa ya Songea zoezi hilo limefanyika kuanzia Agosti 17 hadi 21 mwaka huu katika mitaa yote 95 ya manispaa hiyo kwa walengwa wenye umri wa miaka 5 na kuendelea.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mwampamba amesema zoezi hilo limefanyika kwa kaya 76,843 zilizopo ndani ya Manispaa ya Songea.



Baadhi ya majengo katika hospitali ya Mpitimbi wilayani Songea

# RUVUMA YAFANYA TATHMINI YA MKATABA WA LISHE



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, wadau wa lishe pamoja na Taasisi binafsi, imefanya tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe na programu jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ngazi ya Mkoa kwa mwaka 2023/2024

Mgeni rasmi kwenye kikao cha tathmini hiyo kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea alikuwa ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma aliyewakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Songea,Mheshimiwa Kapenjama Ndile.

Mkuu wa Mkoa ameitaja lishe bora kuwa ni silaha ya kupambana na maradhi, ambayo ni adui wa Taifa ndiyo maana tathmini ya lishe inafanyika kila robo ya mwaka kutokana na umuhimu wake

"Katika kupambana na adui maradhi, silaha mojawapo muhimu sana ni lishe. huwezi kupambana na maradhi katika Taifa kama lishe ya watu wako ni duni," amebainisha

Ameongeza kuwa suala la malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto linaenda sanjari na lishe, kwa kuwa kuboresha lishe kunapunguza uwezekano wa maradhi katika jamii na kuimarisha afya za watoto.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Nyasa,Mheshimiwa Peres Magiri, amesema kumekuwa na maendeleo mazuri kimkoa katika upande wa lishe na kwamba wilaya ya Nyasa inafanya juhudi kubwa kuhakikisha mkataba wa lishe unatekelezwa.

Ameitaja wilaya hiyo inafanya vizuri katika suala la lishe, ikinufaika na uwepo wa ziwa Nyasa linalowezesha upatikanaji wa samaki wanaotumika kutengeneza lishe

Hata hivyo, amesema bado kuna changamoto katika chakula kinachopelekwa mashuleni kwa ajili ya wanafunzi,ambacho kina ukosefu wa virutubisho ambapo ameahidi kulishughulikia suala hilo kwa kununua mashine ambazo zitaongeza thamani katika uandaaji wa lishe

## MILIONI 276 ZANUNUA MASHINE YA KISASA YA MENO HOMSO



Hii ni mashine mpya ya kisasa ambayo itatumika kutolea huduma za kinywa na meno (Dental 3D Cone Beam Computed Tomography Scan) katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea.

Mashine hiyo imegharimu zaidi ya shilingi milioni 276, fedha ambazo zimetokana na makusanyo ya mapato ya ndani ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea.

## NAIBU WAZIRI WA NISHATI AZINDUA KITUO CHA MAUZO YA MAKAA YA MAWE MBINGA



Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga amezindua kituo cha mauzo ya makaa ya mawe kinachomilikiwa na Kampuni ya Marketing Insight Limited MilCoal kilichopo katika Kijiji cha Paradiso Kata ya Ruanda Wilayani Mbinga Mkoani Ruvuma.

Mhe,Kapinga amesema kuwa Sera ya Nishati na Sera ya Madini zinatambua michango ya Kampuni kwenye maeneo mbalimbali Nchini ili kuhakikisha Wananchi wanaozunguka Kampuni hizo wananufaika nazo.

Katika hatua nyingine Mheshimiwa Judith Kapinga amesema kuwa uwekezaji uliofanywa na Kampuni ya MILCOAL unasaidia ongezeko la ukuaji wa uchumi pamoja na fursa za ajira nchini.

Hata hivyo amesema kutokana na hitaji la umeme katika mgodi wa MILCOAL Naibu Waziri wa Nishati amesema TANESCO wanatarajia kufikisha umeme hivi karibuni kwa gharama ya shilingi milioni 280.

Naye Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Peresi Magiri , akitoa salamu za Mkoa, ameipongeza Kampuni ya MILCOAL pamoja na kampuni mbalimbali zilizopo katika maeneo hayo,pia amewakaribisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika Mkoa wa Ruvuma.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Ruanda Dougras Mwingira amewapongeza wamiliki wa mgodi huo akisema kuwa kuwepo kwa mradi huo kumeleta fursa kwa Wananchi wa Kijiji hicho kwa kukuza fursa ya uchumi kwa wakazi wa kata hiyo.

Mussa Haji ni Mwakilishi wa Kampuni ya MILCOAL amesema kampuni hiyo imefanikiwa kufanya mauzo ya tani laki 330,000 huku wakichangia kiasi kikubwa katika utoaji wa ajira kwa wakazi wa maeneo jirani na Mgodi huo.

## UTALII WA UTAMADUNI UNAVYOCHANGIA KUKUZA UTALII NYASA



Utalii wa utamaduni ni eneo lingine ambalo linachangia sana kukuza utalii wa mahali popote,Watu walioishi miaka mingi iliyopita Wilaya ya Nyasa walicheza ngoma mbalimbali zikiwa na lengo la kuburudisha, kuelimisha, kukosoa au kuwapongeza watu mbalimbali waliofanya mambo mazuri kwa jamii.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa na Naibu Waziri wa Uwekezaji,Viwanda na Biashara Mhandisi Stella Manyanya anataja moja ya ngoma hizo ni Mganda,ngoma hii ilichezwa na wanaume na ngoma ya Kioda ambayo walicheza akina mama.Ngoma nyingine kama vile Lindeku, Mhambo, Lingoga na Chomanga walicheza mchanganyiko wanaume na wanawake.

Anasema katika utamaduni jamii za Nyasa zilialikwa kucheza ngoma za jadi nchi jirani za Msumbiji na Malawi, jambo ambalo hadi sasa bado linadumishwa la watanzania kualikwa kucheza ngoma Msumbiji au wa Msumbiji kualikwa Tanzania hasa vijiji vya mpakani kama vile Chiwindi.

Vyakula ni sehemu kubwa ya utalii,vyakula vya asili kwa wakazi wa Nyasa vimegawanyika katika makundi yafuatayo; chakula kikuu ni ugali wa muhogo, mahindi, ulezi, mtama na ngano, vitoweo vimegawanyika katika makundi manne yafuatayo ambavyo ni samaki wakubwa na wadogo Pamoja na na dagaa.

Kundi la pili ni mboga za majani ikiwemo mlenda, kisamvu, mchicha asili (libonongo), kundi jingine ni wadudu kumbikumbi, likungu, chenene (makururu), viyenje,mbambwa (majimoto) na manganiwa.

Wilaya ya Nyasa pia ina pori ya akiba la wanyamapori la Liparamba ambalo lina wanyama wengi wakiwemo tembo, simba, chui, nyati, ngolombwe, parahala, tandala wakubwa, pundamilia, nyani manjano, pongo, Ngiri, pofu, kuro, fisi, nguruwepori na ndege jamii mbalimbali zaidi ya aina 80 ambao ni kivutio kizuri kwa watalii.

Wanyamapori hao wa Liparamba katika majira fulani ya mwaka wanatabia ya kuhama kwenda nchi jirani ya Msumbiji na baadaye hurudi tena kwenye pori la Liparamba kwa kuwa eneo hilo ni ushoroba wa wanyamapori.

Liparamba pia ni pori lenye maporomoko ya maji ya mto Ruvuma ambao umepita humo na unapokea maji kutoka mito miwili ya Lunyele na Lumeme ni kivutio kikubwa cha utalii na uwekezaji katika sekta.

Wilaya ya Nyasa ili iendelee kuwa kitovu cha utalii mkoani Ruvuma,uongozi unaendelea kulinda maeneo ya kihistoria na kiutamaduni kwa kushirikisha wananchi.




Serikali imetanua na kukarabati uwanja wa ndege wa Songea kwa gharama ya Zaidi ya shilingi bilioni 37 ambapo hivi sasa safari za ndege zimeongezwa kutoka mara tatu hadi mara nne kwa wiki

## WAKULIMA NAMTUMBO WATAJA CHANGAMOTO YA KUKOSA ELIMU KWENYE MAHINDI



WAKULIMA wa mahindi wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma,wameitaja changamoto ya kukosa elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo ikiwemo mbegu bora na mbolea kutoka kwa maafisa ugani hali iliyosababisha kuzalisha mazao yasiyo kidhi viwango kulingana na mahitaji ya soko la Serikali.

Wamesema hayo,wakati wa kazi ya uuzaji na ununuzi wa zao la mahindi unaofanywa na Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya chakula(NFRA) katika kituo cha Rwinga wilayani humo.

Faraji Abed amesema,wakulima wako tayari kuzalisha,lakini elimu ya uzalishaji wa mazao bora ni kikwazo kikubwa ambacho kimesababisha baadhi ya wakulima kukata tamaa na kushindwa kuendelea na uzalishaji mashambani.

“tunaiomba Serikali maafisa ugani tuwe nao mashambani ili sisi wakulima tusiendelee kupata hasara ya kuchagua mazao yetu pindi tunapofikisha sokoni,kama maafisa kilimo tungekuwa nao kuanzia wakati wa maandalizi ya shamba hadi msimu wa mavuno basi tusingepata hasara kubwa namna hii”alisema Abed.

Amesema,wakulima wana mwamko mkubwa wa kulima,lakini changamoto kubwa

ni kupata mazao yenye sifa ya kufikisha sokoni yakiwa na ubora wake ule ule hali inayopelekea wakulima kuamini kama kilimo ni kazi inayoweza kuwaletea manufaa katika maisha yao.

Ameishukuru serikali kwa kununua mahindi kwa bei ya Shilingi 700 kwa kilo moja ikilinganisha na bei ya Shilingi 350 ya wafanyabiashara wa mitaani ambayo haikidhi mahitaji na gharama za uzalishaji.

Mkazi wa kijiji cha Rwinga Salum Idd,ameishukuru Serikali kuwaletea kituo cha ununuzi wa mahindi,lakini changamoto kubwa wanatumia muda mrefu kusafisha mahindi kabla ya kupokelewa.

Amesema,hali hiyo imetokana na uzembe wa maafisa ugani ambao hawakwenda mashambani kuwapa elimu ya kilimo cha kisasa hasa katika matumizi ya mbegu bora na mbolea.

## WAKULIMA WA MAHINDI KIGONSERA WASISITIZWA KUZINGATIA USAFI



Baadhi ya wakulima wa mahindi wa kata ya Kigonsera Halmashauri ya wilaya Mbinga mkoani Ruvuma,wakimsikiliza Meneja wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula(NFRA)Kanda ya Songea Zenobius Kahere (hayupo pichani) kuhusiana na utaratibu mpya wa ununuzi wa mahindi ambapo mkulima anatakiwa kuyafanyia usafi na kuchambua mahindia mabovu kabla ya kupima.



WAKULIMA wa mahindi mkoani Ruvuma,wamekumbushwa umuhimu wa kufuatilia maendeleo ya mazao yao mashambani na kuhakikisha wanavuna mazao yaliyokomaa ili kupata soko la uhakika.

Wito huo umetolewa na Meneja wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya chakula (NFRA) Kanda ya Songea Zenobius Kahere, wakati akizungumzia maandalizi ya ununuzi wa mahindi katika msimu wa kilimo 2024/2025 ofisini kwake mjini Songea.

Amesema,hatua hiyo itawezesha NFRA kupata nafaka bora kwa ajili ya akiba ya chakula kwa wananchi watakaopatwa na upungufu wa chakula katika maeneo yao.

## WAKULIMA WA MBAAZI TUNDURU WAUZA KILO 2,478,000



WAKULIMA wa zao la mbaazi wa Wilaya ya Tunduru mkoa wa Ruvuma, wameuza jumla ya kilo 2,478,000 katika mnada wa kwanza uliofanyika katika Chama cha msingi cha Ushirika Chichilimbe kata ya Mbesa.

Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru TAMCU Marcelino Mrope amesema,mbaazi hizo zimeuzwa kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye vyama vya msingi vya ushirika ambapo bei wastani ni Sh.1,986 kwa kilo moja.

Mrope amesema,Chama kikuu cha Ushirika katika msimu wa masoko 2024/2025 kitaendelea kuuza mbaazi kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, na ununuzi hautakuwa kama hapo awali ambapo wanunuzi walikuwa wanaweka barua katika masanduku siku moja kabla ya mnada.

Kwa mujibu wa Mrope,ununuzi wa mbaazi na mazao yote yaliyoingizwa kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani katika msimu wa mwaka huu, uendeshaji wa masoko yake utasimamiwa na Soko la bidhaa Tanzania(TMX)na minada yote itaendeshwa kidijitali.

Ametaja makisio ya uzalishaji wa zao la mbaazi yaliyofanywa na Chama hicho kupitia vyama vya msingi vya Ushirika(AMCOS) msimu wa kilimo 2024/2025 ni

kuzalisha kilo 7,050,000.0 ambazo ni ongezeko la kilo 1,991,194 za msimu uliopita.

Katika msimu 2023/2024 Chama kikuu kiliendesha minada mitano ambapo jumla ya kilo 5,058,806.0 za mbaazi zenye thamani ya Sh.bilioni 10,162,065,952.00 ziliuzwa.

## MALORI 120 HUBEBA MAKAA YA MAWE KWA SIKU MGODI WA JITEGEMEE MBINGA




Meneja Uchimbaji wa kampuni ya Mgodi wa Makaa ya Mawe ya JITEGEMEE Wilayani Mbinga Mkoani Ruvuma Bosco Mabena amesema malori zaidi ya 120 hubeba makaa ya mawe kwa siku katika mgodi huo na kwamba uzalishaji wa madini hayo unafanyika kwa njia za kisasa.

Mabena amesema hayo wakati anatoa taarifa ya uchimbaji madini ya makaa ya mawe kwa viongozi kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ambao wapo mkoani Ruvuma kwenye kampeni ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani na usajiri wa biashara TIC.

Amesema makaa ya mawe yanayozalishwa kwenye mgodi wa Kampuni ya JITEGEMEE hutumika katika viwanda vilivyopo ndani ya nchi,Afrika Mashariki na nchi za Ulaya na China.

“Huu ni mgodi wa kitanzania ambao unaendeshwa na wazawa kwa asilimia 100,tunavyo vitalu vya makaa ya mawe ambavyo vinachimba makaa ya mawe kwa njia ya kisasa kwa sababu tuna vifaa vya kisasa vikiwemo maabara ya kisasa na mitambo ya kuchakata makaa ya mawe kwa ubora wa hali ya juu’’,alisisitiza Mabena.

Amesema makaa ya mawe yanatumika katika viwanda mbalimbali vikiwemo vya saruji katika mikoa mbalimbali nchini,pia amesema makaa ya mawe yanatumika katika viwanda vya tires,nondo na viwanda vyote vidogo vidogo vikiwemo viwanda vya nguo ambapo amesema wanapakia makaa ya mawe bandari ya nchi kavu zaidi ya 120 kwa siku.

Hata hivyo amesema Kampuni ya JITEGEMEE ina ghala la kutunzia makaa ya mawe katika bandari ya Mtwara lenye uwezo wa kutunza makaa ya mawe zaidi ya tani laki tano kwa ajili ya kuuza katika masoko ya nje ya nchi kupitia bandari ya Mtwara.

Kwa upande wake Meneja Uhamasishaji Uwekezaji wa Ndani Kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) Felix John ameipongeza Kampuni ya JITEGEMEE kwa uwekezaji mkubwa ambapo amesema TIC imefika mkoani Ruvuma kwa lengo la kutembelea miradi ya uwekezaji wa wazawa katika Mkoa wa Ruvuma iliyosajiriwa kupitia TIC.

Amesema TIC ipo mkoani Ruvuma kwa lengo la kutoa elimu ya uwekezaji wa ndani na usajiri wa miradi katika kituo cha TIC ambapo amesisitiza kuwa wanaamini wananchi wa Mkoa wa Ruvuma watajitokeza kwa wingi kusajiri miradi yao ili waweze kunufaika na vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi vinavyotolewa na serikali kupitia TIC.

Kwa upande wake Afisa Biashara wa Mkoa wa Ruvuma Joseph Kabaro amesema bado Mkoa una fursa nyingi za uwekezaji katika sekta ya madini kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma umebarikiwa kuwa na aina mbalimbali za madini.

Ameyataja madini hayo kuwa ni makaa ya mawe,dhahabu,chuma,uranium,madini ya vito, shaba na madini ya ujenzi ambapo amesema hadi sasa kampuni zilizojitokeza kuchumba makaa ya mawe ni 18.

Madini ya Makaa ya mawe katika Mkoa wa Ruvuma yanachimbwa katika wilaya za Songea,Mbinga,Nyasa na Namtumbo.

Kituo cha Uwekezaji Tanzania katika Mkoa wa Ruvuma kimeweza kuwatembelea wawekezaji wazawa wawili ambao ni Kampuni ya SUPEFEO ya mjini Songea na Kampuni ya Uchimbaji madini ya JITEGEMEE wilayani Mbinga.

## UTALII NYASA UNAANZIA NA JINA MBAMBABAY



Mbambabay ni mji ambao ni makao makuu ya wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma,

kulingana na Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe jina la "Mbamba bay," ni kwamba Mbamba lina maana ya radi na bay ikimaanisha ghuba.

Mbambabay ni Kitovu cha utalii mkoani Ruvuma kwa kuwa ni mji wenye vivutio vya utalii vya kila aina,vivutio vyenye historia ya kupendeza na kuvutia kwa wageni.

"Tafsiri hizi ambazo zilitolewa na wenyeji zinasema wakati wa zamani kutokana na radi kali za mara kwa mara kupiga kwenye Rasi iliyopo karibu na Ghuba hiyo na ndipo eneo likaitwa Mbamba bay'',anasisitiza Challe.

Challe anabainisha Zaidi kuwa Rasi hiyo ni kubwa na imefunikwa na uoto wa asili wa miti na nyasi, baadhi ya miti hiyo inatumika kama dawa za asili hadi sasa.

Wakazi wa eneo hilo hutumia msitu wa Mbamba kwa matambiko ya kupiga ngoma za kufukuza au kuita majini kwa imani zao na kwamba katika msitu huo kuna wanyama kama chui ambao hutokea milima ya Nangombo, Ukuli na Chinyemba ambao wanapatikana katika rasi hiyo,wakiwafuata wanyama aina ya ngedere waliopo kwa wingi katika msitu huo.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya anataja moja ya ngoma maarufu wilayani humo ni Mganda,ngoma hii inachezwa na wanaume na ngoma ya Kioda ambayo inachezwa na akina mama.

Ngoma nyingine maarufu wilayani Nyasa ni kama vile Lindeku, Mhambo, Lingoga na Chomanga ambazo wanacheza mchanganyiko wanaume na wanawake.

Wachezaji ngoma kutoka Nyasa walialikwa kucheza ngoma za jadi nchi jirani za Msumbiji na Malawi, jambo ambalo hadi sasa bado linadumishwa la watanzania kualikwa kucheza ngoma Msumbiji au wa Msumbiji kualikwa Tanzania hasa vijiji vya mpakani kama vile Chiwindi.

## ZIWA NYASA LINA AINA 600 ZA SAMAKI-UTAFITI



Kulingana na ripoti ya utafiti wa mwaka 2011,asilimia 15 ya aina za samaki wa maji baridi duniani wanapatikana ziwa Nyasa ambapo kuna aina ya samaki tofauti zaidi ya 600,huku kukiwa aina ya samaki wa mapambo zaidi ya 400.

Ndani ya ziwa Nyasa kuna viumbe wengine ambao hawapatikani katika ziwa lolote duniani wanapatikana katika maeneo tofauti ndani ya ziwa Nyasa kutegemeana na aina na usalama wa maisha yao.

Jonathan Ruanda Mtaalam wa kuzamia samaki wa mapambo katika ziwa Nyasa na Mfanyabiashara wa samaki hao anasema tangu mwaka 1960 samaki hai wa mapambo walianza kuuzwa katika nchi za Ulaya na Marekani.

Hata hivyo anasema nchi nyingi kama vile Japani, Sweden, Uturuki, Denmark, Canada, Ufaransa, Uingereza na Ujerumani zilivutiwa na samaki wa mapambo kutoka ziwa Nyasa kutokana na kuwa na sifa ya kipekee yaani rangi nzuri za kupendeza na hakuna sehemu nyingine wanapatikana samaki wa mapambo wa aina hii.

# MWENYEKITI MADABA AWAKUMBUSHA WATUMISHI KUJIBU HOJA



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma Mheshimiwa Teofanes Mlelwa ameongoza kikao cha Baraza la madiwani la Halmashauri hiyo kilichofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Madaba,

Akizungumza kwenye kikao hicho amewakumbusha watumishi kuhakikisha kuwa wanakamilisha kazi ya kukamilisha majibu ya Hoja za CAG kabla ya tarehe ya mwisho na kuwataka watendaji wa kata kwenda kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa ambao unatarajia kufanyika Novemba 27 mwaka huu.



Baadhi ya majengo katika hospitali ya Halmashauri ya Madaba wilayani Songea

# NAIBU WAZIRI WA HABARI ASIKILIZA KERO ZA MAWASILIANO VIJIJI NANE VYA MADABA



Naibu waziri wa Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari Mhandisi Marryprisca Mahundi amefanya ziara ya katika vijiji nane vilivyopo katika Kata nne za Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma kwa lengo la kusikiliza Kero za mawasiliano zinazowakabili wananchi wa maeneo hayo.

Vijiji hivyo ni Igawisenga, Wino, Maweso, Matetereka, Mkongotema, Lutukira, Ndelenyuma na Mbangamawe ambapo vijiji hivyo vipo katika kata za Wino, Matetereka, Mkongotema na Gumbiro.

Ziara hiyo ya Naibu waziri imelenga kusikiliza changamoto za wananchi wa Madaba hususani zinazohusu sekta ya mawasiliano ili kuweza kuzitatua kwani wananchi hao wamekuwa wakisumbuliwa na uwepo wa mawasiliano hafifu mara kwa mara hali inayokwamisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuathiri huduma nyingine za kijamii.

Amesema Wizara ya Habari inakusudia kufungua kituo cha redio Jamii katika Halmashauri ya Madaba ili wananchi waweze kuitumia redio hiyo katika shughuli mbalimbali ndani ya Halmashauri ya Mdaba na kupata taarifa za kitaifa na kimataifa kwa urahisi kwa kuunganishwa na redio hiyo.

Katika ziara hiyo Naibu waziri amebainisha juhudi zinazofanywa na Serikali kuhakikisha maeneo ya pembezoni na nchi nzima zinaimarika katika sekta ya mawasiliano ili kuweza kwenda sambamba na uchumi wa kidijitali na mabadiliko ya teknolojia

"Namna ambavyo mnapata mawasiliano ya kusuasua, haimfurahishi Mheshimiwa Rais ametutuma kutoka wizarani tuhakikishe tunapita, tunajionea, tunaongea na nyie mwisho wa siku tunakuja kuimarisha mfumo wa mawasiliano" ameeleza

Naye Mhandisi Shirikisho Mpunji kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) amesema walitarajia kuwa mnara uliopo eneo la Lilondo kata ya Madaba ungewezesha Mawasiliano maeneo ya vijiji vya Madaba lakini hali ya kijiografia imeathiri uwezekano huo na hivyo maeneo hayo yanahitaji minara mingine

Amebainisha kuwa Wizara imeandaa mradi kwa ajili ya kujenga minara 636 nchini ambapo kati ya minara hiyo, mitano itajengwa katika kata tano za Halmashauri ya Madaba ili kutatua changamoto za mawasiliano zinazowakabili wananchi katika maeneo hayo

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imelenga Kuwezesha utoaji wa huduma za uhakika na za gharama nafuu za Habari, Teknolojia ya Habari, Mawasiliano ya simu na Posta kwa kuweka mazingira yanayokuza ubunifu katika kuibadilisha Tanzania kuwa na Uchumi wa Kidigitali

## BADO VIJIJI VIWILI TU KATI YA 554 RUVUMA KUPATA UMEME



wananchi wametakiwa kulinda miundombinu ya umeme kwa kuepuka shughuli za uchomaji moto kwenye maeneo ya mashamba yao ambayo yamezunguka nguzo za umeme kwani kwakufanya hivyo kunaweza kuathiri kukosekana kwa huduma ya umeme katika maeneo mengine

Wito huo umetolewa na Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga, Mara baada yakuwasha umeme kwa mara ya kwanza katika kijiji cha Mpingi Kata ya Matimila Halimashauri ya Songea

Kapinga ameeleza kuwa maendeleo ni hatua na lazima yawe na awamu ambapo hadi hivi sasa kwa Mkoa wa Ruvuma umebakiza vijiji viwili tu kati ya 554 na kwa Tanzania nzima ni chini ya vijiji 151, ili kukamilisha katika hatua ya awali ya kupeleka umeme kwenye ngazi ya vijiji na baadae kusambaza kwenye vitongoji vyote.

Ametumia nafasi hiyo kumtambulisha Mkandarasi Kampuni ya MF ambae hivi karibuni ataanza kutekeleza mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 284 vya Mkoa wa Ruvuma.

Akizungumza awali wakati akitoa taarifa kuhusu mradi huo wakupeleka umeme katika kijiji hicho cha Mpingi Kata ya Matimira , Mhandisi Kutoka REA Robert Dulle, ameeleza kuwa mradi umegharimu takribani milioni 149 mpaka kukamilika kwake huku akitoa wito kwa wakazi wa eneo hilo wajitokeze kwa wingi kuunganishiwa umeme.

.




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akizungumza kwenye hafla ya Kusaini mikataba ya matengenezo ya barabara Mkoani Ruvuma iliyofanyika Katika viwanja vya ofisi ya MKuu wa Mkoa mjini Songea

## WAZIRI JENISTA MHAGAMA AKABIDHIWA OFISI



Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amekabidhiwa rasmi ofisi na aliyekuwa Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu.

Shughuli ya makabidhiano ya ofisi imefanyika katika Ofisi za Wizara katika Mji wa Serikali, Mtumba, Dodoma.

Mhe. Jenista amempongeza Mhe. Ummy Mwalimu kwa uongozi wake ndani ya Wizara ya afya kwa kipindi chote alichofanya kazi ndani ya Sekta ya Afya kwa miaka 14.

“Nakupongeza Mhe. Ummy Mwalimu hakika maendeleo haya ya Sekta ya Afya una mchango mkubwa katika kuifikisha Sekta ya Afya hapa ilipo, tutaendelea kushirkiana na kupeana ushauri zaidi katika kazi” amesema Waziri Mhagama.

Akikabidhi Ofisi Mhe. Ummy Mwalimu amempongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Waziri wa Afya.

“Umekuwa Kiongozi mwenye uzofu wa kutosha ndani ya Serikali naamini kwa uwezo wako ulionao pamoja na timu hii ya Wizara unaweza kuendelea zaidi katika kuboresha Sekta ya Afya nchini” amesema Mhe. Ummy Mwalimu.

Viongozi wengine wageni walioshiriki kwenye shughuli hiyo ni Naibu Katibu Mkuu Bw. Ismail Rutamila ambaye pia ameahidi kutoa ushirikiano kwa Menejimenti na Viongozi katika kuboresha Sekta ya Afya nchini pamoja na Dkt. Irene Isaka, Mkurugeni Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima.

## TIC YATOA SEMINA KWA WAFANYABISHARA NA WAJASIRIAMALI



Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimetoa semina elekezi kwa wafanyabiashara,wajasirimali na wawekezaji wa Mkoa wa Ruvuma iliyofanyika Katika ukumbi wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania tawi la Songea.

Semina hiyo imelenga kuwahamasisha wawekezaji kusajili biashara zao sambamba na kufahamu fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo ndani ya Mkoa wa Ruvuma na nchini kwa ujumla

Akizungumza kwenye ufunguzi wa semina hiyo,mgani rasmi katibu Tawala wa wilaya ya Songea Mtela Mwampamba ameishukuru TIC na Serikali kwa ujumla kwa juhudi za kuhakikisha inaandaa mazingira rafiki ya uwekezaji ndani ya Mkoa wa Ruvuma.

Amesema katika kuboresha miundombinu ya barabara mjini Songea kwa lengo la kuvutia wawekezaji,Manispaa ya Songea imepokea zaidi ya bilioni 22 za matengenezo ya barabara 22 kwa kiwango cha lami nzito.

Ameongeza kuwa pia serikali imetoa shilingi bilioni 19 za ujenzi wa masoko mawili ya kisasa mjini Songea pamoja na kuboresha sekta ya viwanda ikiwa ni juhudi za Serikali kuboresha shughuli za uwekezaji nchini

"Tumeshaletewa pesa zaidi ya bilioni 22 kuhakikisha ndani ya manispaa barabara zote zinakuwa za lami, lakini kwa kutambua kwamba watu wa Ruvuma ni wawekezaji wakubwa, tayari tumeshapokea shilingi bilioni 19 ili tuweze kujenga masoko mawili ya kisasa mjini Songea" Amebainisha

Naye Afisa Biashara Mkoa wa Ruvuma Joseph Martin Kabalo amezitaja fursa mbalimbali za uwekezaji zinazopatikana ndani ya Mkoa wa Ruvuma ikiwemo ujenzi wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo, fursa ya uuzaji wa bidhaa za viwandani, utalii, uvuvi na fursa ya usindikaji wa mazao mbalimbali hususani mahindi

Felix John ni Meneja Uhamasishaji Uwekezaji wa Ndani kutoka TIC amesema wapo Mkoani Ruvuma wakitekeleza kampeni ya uhamasishaji uwekezaji wa ndani ambapo wametembelea miradi miwili ya wawekezaji wazawa wa ndani ya Mkoa wa Ruvuma.

Ameitaja miradi hiyo ni ya mwekezaji SUPERFEO aliyewekeza mradi wa kiwanda cha unga eneo la Namanditi mjini Songea na mradi wa uchimbaji wa makaa ya mawe unaofanywa na kampuni ya wazawa ya JITEGEMEE wilayani Mbinga.

Amesema TIC inatoa elimu endelevu ya uwekezaji na kuhamasisha usajili wa miradi ili wawekezaji waweze kunufaika na vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi vinavyotolewa na Serikali.



Mradi wa mgodi wa makaa ya mawe wa Jitegemee wilayani Mbinga

# UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA KUFANYIKA NOVEMBA 27,2024




WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa amebainisha kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa utafanyika Novemba 27 mwaka huu.

Mchengerwa ameyasema hayo jijini Dodoma wakati wa kutoa Tangazo la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024 ambalo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara 145 na 146 inaelezea uwepo wa Serikali za Mitaa ukilenga kupeleka madaraka kwa wananchi.

Uchaguzi wa mwisho wa Serikali za Mitaa ulifanyika Novemba 2019.

Alisema viongozi wanaochaguliwa katika ngazi hizi ni wenyeviti wa vijiji, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, wenyeviti wa mitaa, wajumbe wa kamati za mitaa na wenyeviti wa vitongoji.

Mchengerwa ametoa tangazo la uchanguzi kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019 ibara 4(1-3) (Matangazo ya Serikali Na. 571, 572, 573 na 574) ya mwaka 2024.

“Hivyo ninautangazia umma wa Watanzania na vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu kuwa tarehe 27 Novemba, 2024 itakuwa ni siku ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara.”

“Upigaji wa kura utaanza saa mbili kamili asubuhi na kumalizika saa kumi kamili jioni. Hivyo ninawatakia uchaguzi mwema, amani na utulivu katika kipindi chote cha uandikishaji, uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji kura, wakati wa kutangaza na kupokea matokeo ya uchaguzi.”

Aidha, Mchengerwa alisema utauzie wa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo utafanyika Septemba 19 hadi 25 mwaka huu, wakati uandikishwaji wa wapigakura utafanyika kati ya Oktoba 11 hadi 20 mwaka huu.

Alisema uteuzi wa wagombea utafanyika Novemba 8 mwaka huu wakati kampenzi zimepangwa kuanza Novemba 20 hadi 26 mwaka huu.

Alisema alisema wagombea wa nafasi za uongozi watatakiwa kuwa wanachama na wadhamininiwa wa Vyama vya Siasa vyenye Usajili wa Kudumu.

“Mgombea au mtu aliyeomba kuteuliwa anaweza kuweka pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea.”

Mchengerwa alisema nafasi zote zinazogombewa zilikuwa na uongozi kwa kipindi cha miaka mitano na viongozi walioko madarakani uongozi waon utakoma siku saba kabla ya siku ya kuchukua fomu za kugombea uongozi.

“Pia kura zitapigwa katika namna itakayozingatia usiri na kwa kutumia karatasi maalum za kupigia kura ambazo zitatakiwa kutumbukizwa katika masanduku maalum ya kupigia kura.”

Hata hivyo vyama 18 kati ya 19 vyenye usajili wa kudumu vimeshiriki hafla hiyo na kukabidhiwa kanuni za uchanguzi ispokuwa Chadema ambao hawakuwa na mwakilishi



## RC RUVUMA AFANYA MAZUNGUMZA NA KAMISHINA WA TIRA




Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo Saqware akiambatana na ujumbe wake wamekutana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed

Zoezi hili ni mkakati endelevu wa ziara ya kuwatembelea Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ili kuhakikisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) inaendelea kuwafikia watanzania kwa kutoa elimu na kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya bima na hatimaye wawe watumiaji wazuri wa huduma na bidhaa za bima ili na wao wawe mabalozi kwa wengine.

Ruvuma ni mkoa wenye Wilaya tano zikiwemo Songea, Tunduru, Namtumbo, Mbinga na Nyasa na jumla ya Halmashauri nane. Huu ni moja ya mkoa Kusini mwa Tanzania wenye fursa nyingi za uwekezaji katika kilimo, uvuvi, ufugaji, uchumbaji wa madini na utalii. Kutokana na uwepo wa shughuli hizi za kiuchumi zinazochochea maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma na mikoa mingine ya jirani inayojumuisha Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ni vema shughuli hizo, watu na mali zao wakapewa kinga ya bima.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) imetumia fursa hiyo kuzungumza na kutoa elimu ya bima kwa watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kuwawezesha na kuwajengea uelewa wa masuala mbalimbali yanayohusu bima ili nao waweze kuwa watumiaji wa bidhaa na huduma za bima na badae wawahamasishe Wanaruvuma.

Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo Saqware ameeleza kuwa Tira inatekeleza mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa (FYDP II-2020-2025) pamoja na

Mpango Mkuu wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Nchini (FSDMP-2020-2030) amabo unawataka watanzania wote kushiriki kwenye mpango huo kwa kuwa watumiaji na kuwa mabalozi kwa wengine.

Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed ameisisitiza sekta ya bima kuzingatia viwango vya utoaji wa huduma za bima kwa watanzania. Amesema kuwa muonekano wa miundombinu wa kutolewa huduma ikiwemo ofisi za watoa huduma za bima hususan kwa wakazi wa Ruvuma iboreshwe ili kuweka mazingira wezeshi na shawishi kwa wale wanaolengwa ili kuwahudumia kwa ueledi na ufanisi muda wote.

Dkt. Saqware amewahakikishia Wanaruvuma kuwa Mamlaka ipo na itaendelea kuwafikishia huduma za bima zenye tija na zenye manufaa huku soko la bima likibaki kuwa salama na linalosimamiwa kwa ueledi mkubwa.

## MJI WA PERAMIHO UNAVYOUTANGAZA MKOA WA RUVUMA KIMATAIFA



**Mji** wa Peramiho uliopo Wilaya ya Songea Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa miji ya zamani yenye historia ya kipekee katika ukanda ya kusini.

Mji wa huo unafahamika zaidi nje ya nchi pengine kuliko miji mingine iliyopo kusini mwa Tanzania kutokana na mji huo kuwa na historia ya namna yake kipekee ikiunganisha Tanzania na mataifa ya Ulaya.

Historia ya mji wa Peramiho uliopo kilometa 24 tu kutoka makao makuu ya mkoa wa Ruvuma Songea inaunganishwa na wabenediktini wa kanisa katoliki kutoka

St.Otilia nchini Ujerumani, ambao waliamua kuweka makao makuu yao katika Abasia ya Peramiho.

Wabeneditine hao waliingia kwa mara ya kwanza katika mji huo mkongwe mwaka 1898 wakiongozwa na Kasian Spiss. Tangu wakati huo wabenediktine hao wamekuwa wakifanya mambo yanayoutangaza mji huo hali iliyosababisha kuutambua mji wa Peramiho kuwa ni mji unaokidhi vigezo kuwa mji wenye utalii wa kiutamaduni.

Mhifadhi Kiongozi wa Makumbusho ya Taifa Philipo Maligisu anasema wabenediktine wa Abasia ya Peramiho wametengeneza historia ya kipekee na kuvutia katika nchi ya Tanzania ambao wameacha historia katika mji wa Peramiho na taifa kwa ujumla hasa walipojikita katika suala zima la elimu na kuamua kuwekeza katika elimu kwa zaidi ya miaka 100 iliyopita.

Historia inaonesha kuwa walipoingia kwa mara ya kwanza wabenediktine hao kwa kutambua umuhimu wa elimu waliamua kuanzisha madarasa kwa kufundisha walimu na kufundisha wanafunzi hivyo kufundisha elimu zote mbili yaani elimu ya kiroho na elimu dunia

Kwa msingi huo eneo la Peramiho katika historia ya Tanzania ina historia ya kipekee kwa zaidi ya miaka 100 hivyo kuna ushahidi ambao unaonesha wabenediktine walidhamiria kufanya mambo ya msingi katika mji wa Peramiho na taifa kwa ujumla.

Utafiti uliofanywa katika mji wa Peramiho unaonesha kuwa wabenediktine hao walizindua rasmi mji huo Julai 31,1898 na tangu hapo waliendelea na shughuli zao wakiwa na mahusiano mazuri wakati huo na utawala wa machifu katika eneo hilo.

Hata hivyo mahusiano hayo mazuri baina ya wabenedikitine hao kutoka nchini Ujerumani na machifu ulikuja kuharibika wakati wa vita ya Majimaji ambayo vilianza mwaka 1905 na kumalizika mwaka 1907 na kusababisha padre Fransis Scuss wa Abasia hiyo kuuawa Septemba 9 1905.

Baada ya kumalizika vita hiyo, ilijitengeneza tena historia mpya ya kanisa la Abasia ya Peramiho hivyo kulichukulia eneo hilo kama eneo la kipekee kwa kuzingatia misingi ya sheria ya Tanzania namba 10 ya mwaka 1964 na maboresho yake namba 22 ya mwaka 1979 ambayo inayatambua maeneo yote ya kihistoria kulingana na umuhimu wake katika jamii.

Wananchi wa Ujerumani wanaijua Peramiho pengine kuliko hata sisi watanzania,ndiyo maana kizazi na kizazi wanasafiri kwa gharama kubwa hadi katika mji huo ili kufanya utalii wa kiutamaduni kwa kutembelea katika maeneo mbalimbali ya kihistoria ili kujifunza mambo mbalimbali.

Sera ya Taifa ya utamaduni ya mwaka 1997 ina tamka bayana kuwa eneo lolote la kihistoria linapokuwa limetimiza miaka 100 tayari moja kwa moja linaingia katika urithi wa utamaduni wa taifa.

Kutokana na hali hiyo ukiangalia mji huo wa Peramiho tayari umekidhi vigezo na maeneo yake yote ya kihistoria kuingia katika urithi wa utamaduni wa taifa kwa ajili ya kujifunza elimu na utalii.

## MITI ILIYOGEUKA MAWE INAVYOVUTIA WATALII TUNDURU



Miti adimu duniani ambayo inapatikana wilayani Tunduru mkoani Ruvuma ni miti mawe ambayo ni jamii ya miti ya mitetereka ambayo katika dunia nzima inapatikana katika nchi mbili za Tanzania wilaya za Tunduru na Namtumbo mkoani Ruvuma na nchini Marekani.

Miti hii inapatikana katika kijiji cha Mbati wilayani Tunduru na kijiji cha Likuyu wilayani Namtumbo.

Miti hii ni jamii ya miti ya mitetereka. Mti mawe unaweza kuishi kwa zaidi ya miaka 120 changamoto kubwa inayoikabili miti hiyo ni kushambuliwa na watu wengi hivyo ipo katika hatari ya kutoweka.

Kuwepo kwa kivutio cha miti mawe kunaonesha kuwa ukanda wa kusini mwa Tanzania kuna utajiri wa vivutio vya utalii ambavyo havipatikani sehemu nyingine yeyote nchini hivyo vivutio hivyo vikiibuliwa na kutangazwa vinaweza kufungua fursa za utalii kusini.

# JENISTA MHAGAMA ANAVYOENDELEA KUAMIMNIWA NA RAIS



RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan amemteua Mbunge wa Jimbo la Peramiho Mheshimiwa Jenista Mhagama kuwa Waziri wa Afya kabla ya uteuzi huo Mheshimiwa Mhagama alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera,Bunge na Uratibu.

Hongera wananchi wa Jimbo la Peramiho,hongera wananchi wa Mkoa wa Ruvuma



# SUPERFEO ALIANZA NA MTAJI WA 20,000 SASA NI BILIONEA




Mfanyabiashara maarufu Omary Msigwa maarufu kwa jina la SUPERFEO alitafuta fursa za uwekezaji kutoka mkoani Njombe hadi Songea mkoani Ruvuma.

Anasema alianza biashara rasmi akiwa na umri wa miaka 20 baada ya kumaliza darasa la saba kwa mtaji usiozidi  elfu ishirini (20,000).Superfeo  hivi sasa ni miongoni mwa wawekezaji wakubwa mkoani Ruvuma akiwa na mabasi zaidi ya 50,magari ya mizigo yanayobeba makaa ya mawe,kiwanda cha kusaga unga wa mahindi na biashara nyingine.



# MWENYEKITI WA CCM AKABIDHI VIFAA TIBA HOSPITALI YA NYASA



Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Ruvuma Komred Oddo Mwisho ameipongeza serikali kwa kupeleka vifaa tiba vya kisasa vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.4 katika hospitali ya Wilaya ya Nyasa ili kutatua changamoto, na kuboresha sekta ya afya.

Pongezi hizi amezitoa alipotembelea kwa ajili ya kukagua na kukabidhi vifaa tiba hivyo ambavyo vimepatikana kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa na Shirika lisilokuwa la Kiserikali la Human Bridge la nchini Sweden.



# KANALI ABBAS AFUNGUA KIKAO UKUSANYAJI MAONI DIRA MPYA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed amefungua kikao Cha ukusanyaji wa maoni ya uandaaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 ngazi ya Mkoa kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea

Akifungua kikao hiko MKuu wa Mkoa amebainisha kukaribia ukomo kwa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 ambayo imetekelezwa kuanzia mwaka 2000 na kueleza juhudi za Serikali za kuandaa Dira mpya ya Maendeleo ya mwaka 2025-2050 itakayotumika kwa miaka 25 ijayo.

"Katika hatua hizi za mwanzo Jukumu la kuandaa limekabidhiwa kwa timu kuu ya kitaalam ya Dira ,na Moja ya kazi muhimu ni kushirikisha Watanzania wengi kadri iwezekanavyo katika kupata maoni kuhusu mtanzania, jamii na Tanzania waitakayo ifikapo miaka hiyo ya 2050" ameeleza Mkuu wa Mkoa

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo ameitaja Dira ya Taifa ya ya mwaka 2025 imeundwa na nguzo kuu tano ambazo ni maisha Bora na mazuri, kuwepo kwa mazingira ya amani,usalama na umoja, utawala na uongozi Bora, ujenzi wa jamii iliyoelimika na kupenda kujifunza na kujenga uchumi imara.

Makondo ameyataja mafanikio ya utekelezaji wa Dira ya 2025 ikiwemo kuwezesha nchi kupata mafanikio ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kama vile nchi kuingia katika kundi la kipato cha kati cha chini, kuimarika kwa huduma ya elimu na afya na kuimarika kwa huduma za barabara na miundombinu

Kwa upande wake Katibu wa CCT Mkoa wa Ruvuma, Fulko Hyera ameishukuru Serikali kwa kwa kutekeleza mipango iliyowekwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 katika sekta mbalimbali akishauri uboreshwaji zaidi katika sekta ya Elimu na Afya ili kuimarisha zaidi shughuli za uzalishaji mali na uchumi kwa Dira ya mwaka 2050

Mchakato wa maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 ulizinduliwa na Makamu wa Rais Dkt. Isdor Mpango jijini Dodoma.

## TIRA YATOA ELIMU YA BIMA KWA WATUMISHI WA RS RUVUMA



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imetoa elimu kuhusu masuala ya Bima kwa watumishi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa mjini Songea.

Mafunzo hayo ya Bima ni sehemu ya jitihada za TIRA katika kutekeleza Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa na Mpango Mkuu wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Fedha nchini.

Akizungumza wakati anatoa elimu ya Bima kwenye viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Kamishna wa Bima nchini, Dkt. Baghayo Saqware amesema waamedhamiria kuhakikisha elimu ya bima inawafikia wananchi wengi wa Mkoa wa Ruvuma.

Dkt.Saqware, ameomba ushirikiano kutoka kwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili kuhakikisha elimu ya bima inawafikia wananchi wa Ruvuma na kuwajengea uelewa wa kutumia bima kama kinga mahsusi kwa maisha, afya, na mali zao.

"Tunaomba ushirikiano na ofisi yako ili kuhakikisha elimu ya bima inawafikia wananchi wa Mkoa wako kwa lengo la kujenga uelewa wao wa bima ili wabaini manufaa ya kutumia bima kama kinga mahsusi kwa maisha, afya, na mali zao," amesisitiza.

Amemuomba Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kuwa balozi wa TIRA katika utoaji wa elimu ya bima kwa wananchi na kuwahamasisha kutumia bidhaa na huduma za bima hususan bima za afya na kilimo.

Amebainisha kuwa sekta ya bima ina ongezeko la zaidi ya asilimia 10 kwa kila mwaka kwa watoa huduma za bima sambamba na kufanikiwa kuhakikisha ulipaji wa madai ya Bima kwa wakati kwa asilimia 95 na kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma za bima kwa asilimia 20 hadi kufikia mwaka 2023.

Mamlaka ya usimamizi wa Bima (TIRA) imepewa jukumu la kuratibu mambo yote ya kisera yanayohusu bima ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusimamia shughuli zote za Bima Tanzania Bara na Zanzibar.

## KANALI ABBAS AFUNGA MAONESHO YA NANENANE NGAZI YA MKOA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akizungumza wakati anafunga rasmi maonesho na sherehe za Sikukuu ya walimu Nanenane ngazi ya Mkoa wa Ruvuma ambazo zimefanyika kwenye viwanja vya Amanimakoro wilayani Mbinga.

Kaulimbiu ya mwaka huu ya maadhimisho ya sherehe za wakulima Nanenane ni Chagua viongozi bora wa serikali za mitaa kwa maendeleo endelevu ya kilimo,mifugo na uvuvi.

## NAMTUMBO WASHAURIWA KUONGEZA BIDII KWENYE UFUNDISHAJI



Maafisa Elimu Msingi kutoka Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma wametembelea Shule sita za Msingi ambazo ni;- Mdwema, Utwango, Libobi, Suluti, Kanjele, na Nambalama zilizopo katika Wilaya ya Namtumbo ili kujua hali ya Wanafunzi katika Masomo na mwenendo wa walimu katika Ufundishaji.

Mwalimu Rhoda Mbilinyi ni Afisa Elimu Taaluma Msingi Wilaya ya Namtumbo ametoa wito kwa Walimu kuongeza jitihada kwenye ufundishaji makini wa Mada pia kusaidia wanafunzi katika kutatua changamoto zao na kuhakikisha wanafunzi wanajua kusoma na kuandika ili kuinua taaluma na elimu bora Katika Wilaya ya Namtumbo na Taifa kwa Ujumla.

## MASHIRIKA YASIYOKUWA YA KISERIKALI YANA MCHANGO MKUBWA KIUCHUMI




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ameyataja mashirika yasiyo ya kiserikali kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ngazi ya Taifa na kimataifa

Hayo yamesemwa katika hotuba ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Kapenjama Ndile katika Jukwaa la mwaka la mashirika yasiyo ya kiserikali lililofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea

Ametaja mashirika hayo kuwa ni muhimu katika sekta ya maendeleo sio tu hapa nchini bali pia duniani kote ambapo ameyaasa mashirika yasiyo ya kiserikali kufanya kazi kwa kufuata kanuni, taratibu na miongozo ya serikali ili kufanya kazi bila ya kuvunja sheria

“Mnapotekeleza majukumu yenu zingatieni uwazi, Uwajibikaji, kuripoti kwa wasajili wasaidizi ngazi ya Mkoa na Halmashauri, na kupeleka taarifa ya mpango wa bajeti ya shirika Katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa’’,alisisitiza

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo ameyaomba mashirika yote yasiyo ya kiserikali kuhakikisha yanatambulika na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili kuhakikisha ustawi na usalama wajamii na watanzania kwa ujumla.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali Mkoa wa Ruvuma Aidan Mbilinyi amesema wamejipanga kuhakikisha mashirika hayo yanafuata matakwa ya Serikali ili kuweza kuratibu kazi zao kwa kufuata sheria ,kanuni na taratibu zilizowekwa .

Mkoa wa Ruvuma una mashirika yasiyo ya kiserikali 182 ambayo yamesajiliwa kisheria na mashirika 7 ya nje yanayofanya kazi katika Wilaya na Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma yakijishughulisha na shughuli mbalimbali kama afya, elimu na kilimo.

## MKOA WA RUVUMA UNATOA MCHANGO MKUBWA KWENYE CHAKULA



MKOA wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa michache maarufu nchini inayozalisha chakula na kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa.

Hayo yamesema na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakati wa kufunga maonesho na sherehe za wakulima Nanenane ngazi ya Mkoa wa Ruvuma zilizofanyika katika viwanja vya Amanimakoro wilayani Mbinga.

Amesema chakula kinachozalishwa mkoani Ruvuma licha ya kutumika ndani ya Mkoa ,lakini pia kinatumika nje ya Mkoa na nje ya nchi hivyo kusaidia wananchi kupata kipato na kukuza uchumi.

Hata hivyo amewatahadharisha wananchi kutouza chakula chote badala yake wakumbuke kuweka akiba ya chakula ambacho kitawafikisha katika msimu mwingine wa mavuno.

“Serikali imeongeza bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutoka Bilioni 275 hadi bilioni 295 mwaka huu,imeongeza pia bajeti ya Wizara ya Kilimo kutoka Zaidi ya shilingi bilioni 294 hadi kufikia shilingi Trilioni 1.3,hii yote ni dhamira thabiti ya Mheshimiwa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ya kuinua sekta ya Kilimo,Uvuvi na Mifugo’’,alisema Kanali Abbas.

Katika hatua nyingine,Mkuu wa Mkoa ametoa maagizo mbalimbali kwa watendaji wa Halmashauri na Wilaya yakiwemo kusimamia matumizi sahihi ya vitendeakazi vilivyotolewa na serikali kwa maafisa Ugani,kuhakikisha uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa unafanyika kwa utulivu na amani na kuhakikisha shule zenye maeneo yanayofaa wapande maharage lishe na miti ya matunda ili kusaidia wanafunzi kupata lishe.

Maagizo mengine ni Kamati za Pembejeo ngazi ya Wilaya zihakikishe zinakuwa na vituo vya kusambazia mbolea za ruzuku ya serikali na wataalam wa ufugaji Samaki waendelee kutoa elimu ya utengenezaji chakula cha Samaki na kuandaa mazingira wezeshi ya uwekezaji vyakula vya samaki.

Awali akizungumza kwenye maadhimisho hayo Mkuu wa Wilaya ya Mbinga Mheshimiwa Kisare Makori amesema Zaidi ya asilimia 85 ya wananchi wilayani Mbinga ni wakulima wa mazao ya chakula na biashara.

Makori ameahidi kusimamia kilimo ili Wilaya hiyo iweze kutoa mchango mkubwa katika sekta ya kilimo na kuufanya Mkoa wa Ruvuma kuwa kinara katika uzalishaji wa mazao ya chakula na wananchi waendelee kufaidika kupitia sekta ya kilimo.

Amemuomba Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kulifanya eneo la Amanimakoro kuwa endelevu katika maonesho ya Nanenane ya Mkoa kila mwaka ombi ambalo Mkuu wa Mkoa ameridhia.



# BILIONI 22 KUFANYIA MATENGENEZO BARABARA ZA RUVUMA



WAKALA wa barabara za mijini na vijijini(TARURA) Mkoa wa Ruvuma,kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umeidhinishiwa katumia kiasi cha Sh.bilioni 22,194,409,504.77 kwa ajili ya kufanya matenengezo ya barabara zake.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Silvester Chinengo amesema ,kati ya fedha hizo kutoka Mfuko Mkuu wa Barabara ni Sh.bilioni 7,894,961,998.36 na mfuko mkuu wa serikali wa kila jimbo shilingi shilingi bilioni 4,500,000,000.00 ,fedha za tozo ya mafuta Sh.100 kwa lita ni Shilingi bilioni 9,799,447,506.41.

Chinengo amesema hayo kwenye hafla fupi ya utiaji saini mikataba ya matengenezo ya Barabara iliyoshuhudiwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed mjini Songea.

“mpaka sasa TARURA tumekamilisha manunuzi ya miradi 50 yenye gharama ya Sh.bilioni 14,19,607,702.00 ambapo jumla ya kilometa 1,079 za barabara zitafanyiwa matengenezo ya aina mbalimbali pamoja na ujenzi wa makalavati na madaraja”alisema Chinengo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema ,serikali kupitia TARURA itahakikisha inawalipa Wakandarasi fedha zao ili kuwajengea uwezo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Ameziagiza Taasisi za serikali mkoani humo,kulipa madeni ya wakandarasi kwa wakati ili kuwaepusha wakandarasi kuingia kwenye migogoro mbalimbali ikiwemo kunyang'anywa na kuuziwa mali zao na taasisi za fedha kutokana na fedha walizokopa kama mitaji katika shughuli zao.

Amesisitiza kuwa ,serikali kupitia sekta ya mawasiliano ya barabara imejipanga kuona sekta ya barabara inaimarika ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa mazao kutoka shambani kwenda mijini kwa ajili ya kupata soko la uhakika.

Katika hatua nyingine Kanali Abbas,amezitaka Taasisi za Serikali mkoani humo, kuwapa kipaumbele wakandarasi wazawa na kutoa upendeleo kwa wanawake wanaofanya kazi za ukandarasi ili kuwajengea uwezo na kunufaika na fedha zinazotolewa

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo,amewataka watendaji wa TARURA kuwafuatilia kwa karibu wakandarasi ili miradi inayotekelezwa ikamilike kwa muda uliopangwa na kwa viwango vinavyohitajika.

Naye Mkuu wa TAKUKURU mkoani Ruvuma Hamza Mwenda amesema , TAKUKURU itahakikisha inafuatilia miradi yote iliyopangwa kutekelezwa ili kujiridhisha ubora wa miradi husika.

Mwakilishi wa Wakandarasi wa Mkoa wa Ruvuma Vales Urio kutoka Kampuni ya Ovans Contructions Ltd,ameishukuru serikali kwa kuendelea kuwaamini na kuwapa kazi za ujenzi wa miradi ya barabara na kuhaidi watekeleza miradi hiyo kwa ubora ili kuleta tija kwa mkoa na Taifa.



Daraja la Ruhuhu lililopo katika Mto Ruhuhu unaomwaga maji yake Ziwa Nyasa linaunganisha Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma na Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**

**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**

**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**
**SIMU Nambari.025- 2602256/2602238**
**FAX Na.2602144**
**E-MAIL:** ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
**TOVUTI:www.ruvuma.go.tz**
**INSTAGRAM; rs ruvuma**
**FACEBOOK: rs ruvuma**
**YOUTUBE:rs ruvuma**



# JARIDA LA RS RUVUMA





## TOLEO LA AGOSTI 2024